TANGAZO LA SERIKALI Na………. la tarehe ……………………

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(Sura ya 290)

---

SHERIA NDOGO

---

*Zimetungwa chini ya Kifungu cha 6(1) (b)*

---

SHERIA NDOGO ZA (MASOKO NA UVUVI) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI ZA MWAKA 2016

## SEHEMU YA KWANZA
## MAELEZO YA AWALI

*Jina*

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Halmashauri ya Manispaa ya Lindi (Masoko na Uvuvi) za Mwaka 2016.

*Matumizi na tarehe ya kuanza kutumika*

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika ndani ya mipaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Lindi na zitaanza kutumika mara baada ya kuchapishwa katika gazeti la Serikali.

*Tafsiri*

3. Katika sheria ndogo hizi isipokuwa tu kama itaelekezwa vinginevyo:
"chumba" maana yake ni chumba au jengo lolote linalotumika kuuzia bidhaa ndani ya soko pasipo kuhusisha meza, kizimba au nafasi;
"halmashauri" maana yake ni halmashauri ya Manispaa ya Lindi;
"kodi ya pango"maana yake ni kodi inayolipwa na mpangaji kwa halmashauri kila mwezi au kila siku kwa mujibu wa sheria ndogo hizi;
"mamlaka" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Lindi;
"mkurugenzi"maana yake ni mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, ikiwa ni pamoja na Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri.
"mkuu wa soko"maana yake ni msimamizi wa soko aliyeteuliwa au aliyeajiriwa na Halmashauri;
"mnunuzi" maana yake ni mtu yeyote anayenunua bidhaa au mazao sokoni au katika eneo la mamlaka ya halmashauri;
"mpangaji" maana yake ni mtu yeyote aliyepangishwa chumba, meza au kizimba na halmashauri ndani ya soko au eneo lingine linalomilikiwa na Halmashauri
"muuzaji" maana yake ni mtu yeyote anayeuza bidhaa au mazao katika soko au eneo lililoidhinishwa na mamlaka;
"mvuv" maana yake ni mtu yeyote, kampuni, taasisi au kikundi chochote

kinachofanya, kushughulika au kuhusika na kazi au shughuli ya kuvua samaki, dagaa au mazao mengine ya bahari;

"soko na gulio" ni sehemu maalum iliyotegwa na kumilikiwa na Halmashauri kwa ajili ya biashara ya kuuza na kununua samaki au mazao mengine ya bahari kufuatana na taaratibu zilizowekwa na Halmshauri;
"ushuru wa mazao" maana yake ni ushuru unaopaswa kulipwa kwa kila zao au bidhaa zinazoingizwa ndani ya eneo la mamlaka ya halmashauri;
"vyombo vya kigeni" maana yake ni vyombo vyote vya uvuvi ambavyo makazi yake ni nje ya Mamlaka;
"zao" maana yake ni mavuno ya shambani au maliasili yanayoingizwa kwenye soko au ndani ya eneo la mamlaka.

## SEHEMU YA PILI
## MASOKO

*Upangaji*

4. –(1) Halmashauri itagawanya masoko katika vyumba, vibanda, vizimba au meza kwa ajili ya kupangisha wafanyabiashara kwa utaratibu wa malipo ya siku au mwezi kadiri itakavyoonekana inafaa.
(2) Kila mpangaji wa chumba, kibanda, kizimba na meza atapaswa kuzingatia masharti ya Sheria Ndogo hizi pamoja na miongozo mingine itakayotolewa na Halmashauri pale itakapohitajika.
(3) Upangaji wa vyumba, vibanda, vizimba na meza utakoma kila baada ya miezi kumi na mbili au baada ya upande mmoja wa mkataba kutoa taarifa ya maandishi ya siku 30 kwa upande mwingine ukitoa sababu ya taarifa hiyo na Halmashauri haitawajibika kulipa fidia itakayotokana na taarifa hiyo ya ukomo wa mkataba.
(4) Halmashauri itasitisha mkataba wa upangaji endapo mpangaji atakiuka na/au kukaidi maelekezo ya Halmashauri au kutiwa hatiani kwa kosa chini ya Sheria Ndogo hizi na Halmashauri haitawajibika kulipa fidia ya aina yoyote.
(5) Baada ya muda wa upangaji ndani ya mkataba kumalizika, upangaji mpya utafanyika kwa njia ya zabuni au kwa namna ambayo Halmashauri itaona inafaa.2

*Kodi ya pango*

5. – (1) Kila mpangaji wa chumba, meza au kizimba atahakikisha kwamba analipa kodi ya pango mwanzoni mwa mwezi au siku na viwango vya malipo ni kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza na la Pili la Sheria Ndogo hizi.
(2) Mpangaji yeyote ataruhusiwa kutumia chumba kilichopo sokoni iwapo atakuwa amelipa kodi ya pango ya mwezi husika na kuwa na mkataba hai.

*Kutohamisha upangaji*

6. Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi mpangaji wa chumba, kizimba au meza:
(a) hatapaswa kupangisha au kuhamisha upangaji wake kwa namna yoyote kwa mtu mwingine pasipo ridhaa ya Halmashauri.
(b) hataruhusiwa kuuza au kuhamisha kwa namna yoyote upangaji wa

chumba, kizimba au meza aliyopanga kwa mtu mwingine.

*Chumba, meza na kizimba kisichotumika*

7.-(1) Halmashauri italazimika kusitisha upangaji endapo mpangaji hatatumia chumba, meza au kizimba alichopanga kwa madhumuni ya kufanyia biashara kama ilivyoainishwa kwenye mkataba wa upangaji au maelekezo yatakayotolewa na Halmashauri.
(2) Haitaruhusiwa kwa mtu yeyote kufunga chumba cha biashara kwa madai ya kukitumia kama stoo au matumizi mengine yasiyoainishwa katika mkataba isipokuwa kwa ridhaa ya Halmashauri na kwa maeneo maalumu kama ambavyo Halmashauri itaona yanafaa.

*Ujenzi na ukarabati*

8. Haitaruhusiwi kwa mtu yeyote kufanya ukarabati au marekebisho ya chumba, meza au kizimba pasipo idhini ya maandishi ya Halmashauri.

*Maeneo ya kufanyia biashara*

9. Mfanyabiashara yeyote hataruhusiwa kufanya biashara nje ya chumba, kizimba au meza.

*Mkuu wa soko*

10. Halmashauri itamteua mkuu wa masoko ambaye atakuwa na wajibu wa kusimamia uendeshaji wa masoko yote ya Halmashauri.

*Usimamizi wa masoko*

11. –(1) Bila ya kuathiri Sheria nyingine yoyote, Halmashauri itakuwa na wajibu wa kuanzisha, kusimamia na kuendesha masoko yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.
(2) Kila mfanyabiashara anayefanya biashara sokoni atatakiwa kusajiliwa na Halmashauri.
(3) Mkuu wa soko kwa kushirikiana na Kamati ya Soko wanaweza kufuta usajili wa mtu yeyote aliyesajiliwa endapo mtu huyo ametenda kosa kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi.

*Uteuzi wa wakala*

12.-(1) Halmashauri inaweza kumteua wakala ambaye atawajibika katika uendeshaji wa soko kwa niaba yake.
(2) Wakala atakayeteuliwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi atakuwa na madaraka yote ya kiutendaji kwa mujibu wa mkataba baina yake na Halmashauri.

*Kamati ya soko*

13.-(1) Kutakuwa na kamati ya soko itakayoundwa na wadau wa soko kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.
(2) Wajumbe wa kamati ya soko watakuwa ni mwakilishi mmoja kutoka kwenye kila kikundi cha ushirika ndani ya soko.

*Kazi ya Kamati ya soko*

14. Kazi za kamati ya soko zitakuwa ni:-
(a) kuhakiki biashara na utendaji wa soko;
(b) kuboresha ustawi wa wanachama wa vyama vya ushirika katika soko;
(c) kuhakikisha nidhamu katika shughuli za soko; na
(d) kuinua ustawi wa biashara katika soko.

*Uundwaji wa kamati ya soko*

15. Kamati ya wadau wa soko itaundwa na kamati ndogo zenye wajumbe wanne kutoka miongoni mwa wajumbe wa kamati ya soko ambao ni:-
(a) kamati ndogo ya miundombinu na usafi;
(b) kamati ndogo ya biashara na utawala; na
(c) kamati ndogo ya ulinzi na usalama.

*Mifugo kutoingizwa sokoni*

16. Kwa mujibu wa sheria ndogo hizi hakuna mifugo itakayoruhusiwa kuingia au kuingizwa sokoni isipokuwa jamii ya ndege na wanyama wadogo wadogo kama sungura watakaoletwa sokoni kwa ajili ya kuuzwa.

*Usajiri wa wafanyabiashara*

17. –(1) Wafanyabiashara wote watasajiriwa na Mkuu wa Soko kwa kushirikiana na Kamati ya Wadau wa soko.

*Tahadhari ya Moto*

18. -(1) Pasipo kuathiri kifungu cha (2) hapa chini, mtu yeyote hataruhusiwa kupika chakula, kuchoma nyama au kuendesha shughuli za mgahawa au shughuli yoyote inayohusisha moto ndani ya eneo la soko isipokuwa kwa idhini ya maandishi ya mamlaka.
(2) Hairuhusiwi kwa mtu yeyote yule kuwasha moto ndani ya soko isipokuwa katika vyumba maalumu ambavyo mamlaka itaruhusu.
(3) Hairuhusiwi kwa mtu yeyote kufanya shughuli za udobi ndani ya soko isipokuwa kama amepewa idhini na mamlaka na kwa masharti maalum.

*Muda wa kufanya biashara sokoni*

19. (1) Muda wa kufungua masoko utakuwa ni saa 12.00 alfajiri na kufungwa saa 12.00 jioni kila siku, isipokuwa kwa vyumba au maeneo maalumu yatakayoainishwa kwenye mikataba ya upangaji na mamlaka kama italazimika kufanya hivyo.
(2) Pasipo kuathiri kifungu cha (1) hapo juu, Hairuhusiwi kwa mfanyabiashara au mtu yeyote kuingia au kufanya biashara sokoni wakati soko limefungwa au kabla ya kufunguliwa.
(3) Kamati kwa kushirikiana na Mkuu wa Soko wanayo mamlaka ya kufunga soko kabla ya saa 12.00 jioni kutokana na mwenendo wa shughuli za soko kwa sababu zitakazoainishwa kwa wakati husika.

*Matumizi ya soko*

20. Haitaruhusiwa kwa mtu yeyote:-
(a) kubandika au kubandua tandazo lolote pasipo idhini ya mkuu wa soko;
(b) kuweka au kupeperusha bendera ya chama chochote cha siasa katika eneo la soko;
(c) kuharibu miundombinu ya soko;
(d) kutumia lugha ya matusi katika eneo la soko;
(e) kutupa taka ovyo katika eneo la soko;
(f) kuingiza vifungashio vya majani au katika eneo la soko ; na
(g) kukiuka kanuni za afya kama zinavyotolewa na Serikali au Halmashauri katika nyakati tofauti.

*Wajibu wa kutunza*

21. -(1) Kila mpangaji wa chumba, meza au kizimba atahakikisha

*usafi na kugharamia huduma za sokoni*

kwamba:-

(a) anatunza eneo lake la biashara katika hali ya usafi wakati wote;

(b) anakuwa na chombo maalumu chenye mishikio na mfuniko kwa kuhifadhia taka;

(c) anatupa taka kwenye eneo lililotengwa na mamlaka kwa kutupia taka; na

(d) anagharamia huduma za ulinzi, usafi, maji na umeme kulingana na mahitaji yake.

*Upakuaji mizigo katika masoko*

22. Mazao na bidhaa mbalimbali zitasafirishwa na kuingizwa sokoni kwa kutumia vyombo vya usafiri, kisha mizigo itapakuliwa na vyombo hivyo vitaondoka sokoni ndani ya masaa sita au kadiri atakavyoelekezwa na Mkkuu wa soko.

*Wajibu wa kulipa ushuru*

23.-(1) Litakuwa ni jukumu la kila mtumiaji wa soko kulipa kodi, ada na ushuru wa masoko kwa Halmashauri kama ilivyoainishwa kwenye jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi.

(2) Halmashauri itatoza ushuru wa magari yote yatakayoingia katika eneo la soko na barabara za soko kwa ajili ya kupakia na kupakua bidhaa kama inavyoneshwa katika jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi.

*Utumiaji wa sehemu ya kuhifadhi samaki au nyama*

24. Mtu yeyote atakayetumia sehemu ya kuhifadhi nyama au samaki ndani ya eneo la soko atatakiwa kulipa ushuru wa soko kwa viwango vilivyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi.

*Malipo ya ushuru kwa wakati*

25. Mtu yeyote atakayeshindwa kulipa ushuru kwa muda uliopangwa atalipa ushuru pamoja na tozo la asilimia Hamsini la ushuru anaodaiwa.

*Milango kwa matumizi ya dharula*

26.Kwa mujibu wa sheria ndogo hizi Halmashauri inaweza kuweka milango maalumu kwa ajili ya matumizi ya dharura na hakuna mtu yeyote atakayeruhusiwa kutumia maeneo hayo kwa matumizi mengineyo.

## SEHEMU YA TATU
## UVUVI

*Matumizi ya sumu*

27.-(1) Mtu yeyote hataruhusiwa:-

(a) kutumia sumu kuua au kushika samaki;

(b) kumiliki samaki waliouawa kwa sumu;

(c) kutumia sumu kuua au kudaka samaki;

(d) kumiliki samaki waliouwa kwa sumu; na

(e) kutumia sumu kuua na kutunza samaki pamoja na mazao ya samaki isipokuwa kwa masuala yahusuyo mafunzo na utafiti.

(2) Mtu yeyote ambaye atakaye kwenda kinyume na kifungu kidogo cha (1) hapo juu atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatakiwa

atahukumiwa kifungo kisichopungua miaka saba.

(3) Ili kutambua kama samaki wameuwa kwa sumu Afisa Muidhiniwa atakuwa na mamlaka ya:-
(a) kuchunguza tabia ya samaki aliyevuliwa kwa sumu au kufanya utafiti na kurekodi matokeo kwenye; na
(b) kuchukua kiwango kidogo kwa ajili ya kumpelekea mtu wa maabara kwa ajili ya uchunguzi.

(4) Matokeo yatakayopatikana kama ilivyo kwenye kifungu kidogo cha (3) hapo juu yatatumika mahakamani kama kielelezo cha ushahidi.

*Kumiliki na kutumia vifaa hatarishi*

28.- (1) Mtu yeyote hataruhusiwa kumiliki au kutumia kwa nia ya kuua au kuvua samaki au kuua mazalia ya samaki:-
(a) vitu vya maangamizi;
(b) baruti;
(c) vitu au mchanganyiko wa vitu ambavyo vipo katika hali ya unga, ngumu, au maji ambavyo zitakuwa na uwezo wa kutoa sumu;
(d) kitu chochote kilicho katika hali yeyote ambacho kinazalisha kemikali zenye simu;
(e) kitu chochote cha plastiki kilicho na uwezo wa kulipuka; na
(f) kitu chochote ambacho waziri wa ulinzi na usalama atakitangaza kuwa ni sumu.

(2) Mtu yeyote hatatakiwa kumiliki samaki walio uawa kwa njia ya sumu, baruti au kwa njia yeyote kama ilivyo katika kifungu cha (1) hapo juu.

(3) Mtu yeyote atakayekiuka masharti yaliyopo katika kifungu kidogo cha (1) na cha (2) hapo juu atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatumikia kifungo kisichopungua miaka mitano.

*Wajibu wa kulipa ada, ushuru na leseni*

29.-(1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya huduma, vibali na leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri kama ilivyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi.
(2) Wachuuzi wadogo wadogo wa samaki wanaofanya biashara ndani ya Mamlaka watatakiwa kulipa leseni ya biashara kama ilivyoelekezwa kwenye Sheria Ndogo hizi.

*Uuzaji wa mazao ya bahari*

30. Utakuwa ni wajibu wa wavuvi wote kufanya biashara ya samaki katika masoko ya samaki au katika maeneo mengine kadiri itakavyoelekezwa na Mamlaka kwa nyakati tofauti.

*Usafirishaji wa mazao ya bahari*

31. Mtu yeyote hataruhusiwa kusafirisha mazao ya bahari kabla hajalipia na kupata kibali cha kusafirisha mazao hayo nje ya Mamlaka ambapo atatakiwa kuonesha stakabadhi ya malipo ya ushuru wa kiasi cha samaki alionunua na kusafirisha.

*Vyombo vya kigeni*

32. Vyombo vyote vya kigeni vitakavyotia nanga katika sehemu ya bahari ya Mamlaka vitatakiwa kulipia ushuru kama ilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi

*Kufifilisha kosa*

33. Mkurugenzi wa Halmashauri anaweza kufifilisha kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, iwapo mkosaji atakuwa amekiri kwa maandishi na atalazimika kulipa faini isiyozidi Shilingi Elfu Hamsini tu.

*Kufuta GN. No.60/2016*

34. Sheria Ndogo za (Ushuru wa Masoko) za Halmashauri ya Manispaa ya Lindi za mwaka 2016 zimefutwa.

*Adhabu*

35. Mtu yeyote atakayevunja Sheria ndogo hizi, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atalazimika kulipa faini isiyopungua Shilingi 50,000/= au kutumikia kifungo cha muda usiozidi miezi 12 au vyote kwa pamoja yaani kifungo na faini.

## JEDWALI LA KWANZA

KIBALI CHA KUTUMIA SOKO
*(Chini ya kifungu cha 11(2)*

1. Jina la mwombaji: ……………………………………………………………………………
2. Anuani ya mwombaji: ……………………………………………………………………….
3. Kibali cha:

   …………………………………………………………………………………….
4. Eneo ambalo kibali hicho kitatumika:

   …………………………………………………………………………………….
5. Kibali kitaanza kutumika kuanzia tarehe ………….. hadi ……………….
6. Maharti ya kibali:-

   (a) ……………………………………………………………………………………

   ………………………………………………………………………………

   (b) ……………………………………………………………………………………

   ………………………………………………………………………………

   (c) ……………………………………………………………………………………

   …………………………………………………………………………………

(d) ……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

(e) ……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

7. Namba na tarehe ya muhtasari wa kamati ya wadau iliyoidhinisha kibali: -

   Na. ………………………….. wa tarehe ………………………………

8. Kimesainiwa na:-

   Jina: ………………………………………………………….

   Saini: ………………………………………………………..

   Cheo: ……………………………………………………....

   Tarehe: …………………………………………………..

   Muhuri: …………………………………………………..

**JEDWALI LA PILI**

USHURU WA SOKO
*(Chini ya kifungu cha 23)*

| NA | AINA YA MAZAO | KIWANGO CHA USHURU (Sh) |
|---|---|---|
| 1 | Tenga dogo la nyanya, nyanya chungu, vitunguu, mbogamboga, bamia n.k | 500/= kila moja |
| 2 | Tenga kubwa (kwa Na. hapo juu) | 1,000/= kila moja |
| 3 | Tenga la machungwa, maembe, ndizi matango | 1,000/= kwa kila tenga kubwa<br>500/= kwa kila tenga dogo |
| 4 | Gunia la kilo 100 la viazi, maharage na mchele | 1,000/= kila moja |
| 5 | Kiroba kikubwa (Kilo 100) kwa mazao yote yanayobebwa kwa kiroba | 1,000/= kila kimoja |

| | | |
|---|---|---|
| 6 | Kiriba kidogo (Chini ya kilo 100) kwa mazao yanayobebwa kwa kiroba | 500/= kila kiroba |
| 7 | Matunda makubwa (Tikiti, nanasi na maboga) | 100/= kila moja |
| 8 | Nazi | 10/= kila moja |
| 9 | Mnada wa soko | Bidhaa yoyote itakayouzwa jumla kaika mnada wa soko itatozwa ushuru ya 5% ya bei ya mauzo |

**JEDWALI LA TATU**

USHURU WA MAZAO YA BAHARI
*(Chini ya kifungu cha 23)*

| NA | AINA YA KODI/USHURU | KIWANGO CHA USHURU |
|---|---|---|
| 1 | Minada ya samaki katika soko la samaki | Asilimia Tano (5%) ya bei ya mauzo |
| 2 | Kibali cha kusafirisha mazao ya samaki nje ya Manispaa kwa kilo moja:- | |
| | (a) Samaki wabichi | 150/= kwa kilo moja |
| | (b) Kamba Koche (lobster) hai | 1,000/= kwa kilo moja |
| | (c) Kamba Koche (lobster) waliokufa | 500/= kwa kilo moja |
| | (d) Kamba mti (prawns) | 150/= kwa kilo moja |
| | (e) Pweza (octopus) | 200/= kwa kilo moja |
| | (f) Ngisi (squids) | 200/= kwa kilo moja |

| | | |
|---|---|---|
| | (g) Vyou/Vinyamata (Sea Slug) | 50/= kwa kilo moja |
| | (h) simbi (Shells) | 50/= kwa kilo moja |
| | (i) kaa (crabs) (hai) | 500/= kwa kilo moja |
| | (j) Samaki wa kawaida (ordinary fish) wakavu. | 75/= kwa kilo moja |
| | (k) Mwani (sea weeds) | 50/= kwa kilo moja |
| | (l) Mapezi na midomo ya papa (shark, fins and jaws) | 500/= kwa kilo moja |
| | (m) Makome (sea shells) | 300/= kwa kilo moja |

**JEDWALI LA NNE**

ADA YA LESENI YA UVUVI
*(Chini ya kifungu cha 23)*

| NA | AINA YA CHANZO | KIWANGO CHA ADA/USHURU |
|---|---|---|
| 1 | Kusajili chombo cha uvuvi | 20,000/= |
| 2 | Leseni ya chombo cha uvuvi | 20,000/= kwa mwaka |
| 3 | Leseni ya uvuvi | 20,000/= kwa mwaka |
| 3 | Ushuru wa kutia nanga kwa vyombo vya kigeni. | 4,000/= kwa siku |
| 4 | Ushuru wa mazao yanayoletwa na vyombo kutoka nje:- | |
| | (a) mbao | 100/= kwa mbao |
| | (b) mazao ya bahari | 100/= kwa kilo |

## JEDWALI LA TANO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
SHERIA YA UVUVI, 2003

PICHA

MAOMBI YA USAJIRI WA CHOMBO CHA UVUVI

SEHEMU YA 1 (Ijazwe na mwombaji)

(a) Jina kamili: ……………………………………………………………………..
(b) Kazi: ……………………………………………………………………………..
(c) Anuani ya posta: ………………………………………………………………..
(d) Anuani ya biashara: …………………………………………………………..
(e) Anuani ya makazi: ……………………………………………………………….
(f) Namba ya simu: ……………………………………………………………..
(g) Utaifa: …………………………………………………………………………..
(h) Endapo amepata utaifa kwa kujiandikisha, taja namba ya usajili: ……………………………………………………………………………………….
(i) Umri: ………………………….., Jinsi ………………………………………..

*Mimi/sisi tunaomba usajili wa chombo cha uvuvi kifuatacho:-

(a) Jina la chombo (kama lipo) …………………………………………………
(b) Urefu: ……………………………………………………………………………
(c) Aina ya chombo: ………………………………………………………………..
(d) Uzito: …………………………………………………………………………….
(e) Tarehe ya kutengenezwa: ………………………………………………..
(f) Aina ya uendeshaji *makasia/tanga/injini, n.k: ……………………….
(g) Aina ya injini: …………………………………………………………………….
(h) Nguvu farasi: ………………………., Namba ya Injini ………………..
(i) Jina la bandari: ……………………………………………………………..

Mimi/sisi tunathibitisha kwamba:-

(a) Maelezo yote yaliyotolewa hapo juu ni sahihi kwa kadiri ya ufahamu wangu/wetu na kwamba chombo hicho hakikuwahi kusajiliwa Tanzania bara.
(b) Chombo hicho kinachoombewa usajili kiko salama kwa matumizi ya baharini na kupewa cheti Na. …………………. Kilichotolewa na ………………………………………. tarehe ……………………….. kilichotolewa …………………………………………..

| | |
|---|---|
| ……………………………….. | ………………………………. |
| Tarehe ya maombi | Jina na saini ya mwombaji |

SEHEMU YA 2 (Ijazwe na Mwenyekiti wa kitengo cha usimamizi wa fukwe)

Mapendekezo ya
kukubaliwa/kukataliwwa*:…………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………….………

Jina la mtoa mapendekezo: ……………………………………………………….
Saini: ………………….. Wadhifa ……….……….. Tarehe …………….…….

Muhuri: …………………………………..

SEHEMU YA 3 (Kwa matumizi ya ofisi tu): Itajazwa na Afisa leseni.

(i) Maombi yamekubaliwa/yamekataliwa*: ……………………………….
(ii) Sababu za kukataliwa: ………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………..

……………………………. ……………………….. ……………………….
Jina la Afisa leseni Saini Tarehe

…………………………..
Muhuri

**JEDWALI LA SITA**

USHURU WA MAZAO YA BAHARI
*(Chini ya kifungu cha 23)*

PICHA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
SHERIA YA UVUVI, 2003

MAOMBI YA LESENI YA CHOMBO CHA UVUVI

**1. Maelezo ya chombo.**

Maombi ya chombo cha uvuvi kwa kipindi cha ……………………….. hadi ……………………………. kufuatia usajili wa chombo kifuatacho cha uvuvi:-

Jina la chombo: ……………………………………………………………..
Alama ya chombo cha uvuvi: ……………………….………………….
Aina ya chombo: ……………………………….………………………………
Uzito wa juu: ………………………………………….……………………..

Aina ya uendeshaji *makasia/tanga/injini, n.k: ……………………..……….
Aina ya injini: …………..…………… Namba ya Injini ………………….……..
Urefu wa chombo: ………………………..…………….…………………………..
Jina la bandari: ………………………………………………………………..……..

**2. Maelezo ya leseni ya awali (kama yapo).**
Namba ya leseni: ……………………………………………………………………………
Tarehe na sehemu ilikotolewa: ………………………………………………………………
Tarehe ya mwisho kutumika: …………………………………………………………………

Endapo chombo hakikuwahi kupata leseni, eleza sababu:
………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………..

**3. Maelezo ya mwombaji.**

Jina: ……………………………………………………………………………………..
Anuani ya posta: ………………………………………………………………………..
Anuani ya makazi: ………………………………………………………………………
Namba ya simu: ……………………………. Nukushi ……………………….
Barua pepe: ……………………………………………………………………………
Utaifa: ……………………………………………………………………………………..

Nathibitisha kwamba kwa kadiri ya ufahamu wangu maelezo niliyoyatoa hapo juu ni ya kweli.

Tarehe: ……………………………...

……………………………………………………………..
Jina na saini ya mwombaji

**4. Kwa matumizi ya ofisi tu.**
(Mapendekezo ya Afisa leseni)

(i) Maombi yamekubaliwa/yamekataliwa*: ……………………………….
(ii) Sababu za kukataliwa:
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………..

………………………………. ………………………….. ……………………….
Jina la Afisa leseni Saini Tarehe

……………………………..
Muhuri

*Futa isiyostahili

## JEDWALI LA SABA

FOMU YA KUFIFILISHA KOSA

*(Chini ya kifungu cha 31)*

Mimi ……………………………………………… wa S.L.P. ………., ………………………………….. niayefanya biashara ya ………………………………………………………………….. Ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, nakiri kutenda kosa la …………………………………………………………………. ikiwa ni kinyume na kifungu cha …………….. cha Sheria ya Ndogo za (Masoko na Uvuvi) za Halmashauri ya Manispaa ya Lindi za Mwaka 2016. Kwa hiyo, kwa hiaria yangu mwenyewe pasipo kushawishiwa na mtu yeyote nakubali kulipa faini iliyoainishwaa kwenye Sheria Ndogo hizi iwapo Mkurugenzi atatekeleza madaraka aliyopewa chini ya kifungu cha 31 cha Sheria Ndogo hizi.

Saini: ………………………………………………..

Mbele yangu:-

Jina: ………………………………………………..

Saini: ………………………………………………..

Wadhifa: ………………………………………………..

Sheria ndogo hizi zilipigwa Muhuri wa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi kufuatia maamuzi yaliyopitishwa kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika tarehe 28 mwezi Aprili, 2016 mbele ya:-

J. M. Satura,
*Mkurugenzi wa Manispaa.*

Mohamed L. Lihumbo,
*Mstahiki Meya wa Manispaa.*

NAKUBALI

Dodoma

John Pombe Magufuli,
RAIS.

Tarehe:…………………..